Ulimwengu Katika Siku za Paulo






# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Somo La Kwanza

## UGEUZI KAMILI

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 9:1-25**

Paulo ndiye shujaa tutakayejifunza habari zake katika masomo yote ya kitabu hiki. Wakati tulipokutana na Paulo kwa mara ya kwanza, alikuwa akiitwa Sauli, na aliwachukia sana Wakristo kwa sababu waliamini ya kwamba Yesu ndiye aliyekuwa Mwana wa Mungu. Paulo aliamini Mungu, na alifikiri kwamba hakuna mtu aliyepaswa kusema kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Alifikiri kwamba alikuwa akimsaidia Mungu kwa kuwatesa Wakristo. Katika somo hili tutaona jinsi Paulo alivyogeuka kuwa rafiki mwaminifu wa Wakristo. Tutajifunza jinsi Paulo alivyogeuka kuwa msaidizi wa Bwana Yesu Kristo.

Wafuasi wa Yesu walitafutwa katika mji wote wa Yerusalemu. Walikamatwa na kuwekwa gerezani, tena mara nyingi walipigwa na hata kuuawa. Watawala wa Kiyahudi na viongozi hekaluni hawakumwamini Yesu Kristo kama Mwana wa Mungu. Walitaka kuwaadhibu watu hawa waliojiita Wakristo.

Mmoja kati ya watu wale waliowakamata Wakristo wengi aliitwa Sauli. Sauli alitaka kwenda Dameski kwa sababu alisikia kwamba kulikuwa na Wakristo wengi sana huko. Alipata ruhusu kutoka kwa viongozi wale kwenda kuwakamata Wakristo wa Dameski. Angewafunga Wakristo hawa na kuwarudisha Yerusalemu kuwaweka gerezani. Aliwachukua watu kusafiri pamoja naye ili watu hao wangemsaidia kuwalinda Wakristo wasitoroke.

Alipokaribia mji wa Dameski, nuru kutoka mbinguni ilimwangaza kote. Nuru hiyo iliangaza karibu sana hata ikawaangusha chini Sauli na watu wale waliosafiri pamoja naye.



Nuru hiyo ilipofusha macho ya Sauli. Kisha sauti ikasema, "Sauli, Sauli, mbona waniudhi?" (Matendo 9:4) Sauli aliuliza, "U nani wewe, Bwana?" Sauti hiyo ilimwambia, "Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe."

Sauli alimwuliza Yesu kama alimtaka afanye nini. Bwana alimwambia Sauli kusimama na kwenda katika mji wa Dameski na baada ya kufika huko angemwambia jambo la kufanya. Wale watu waliokuwa pamoja na Sauli walimwongoza mpaka Dameski kwa sababu hakuweza kuona. Alikaa nyumbani mwa Yuda siku tatu, na alikuwa hawezi kula, kunywa, au kufanya jambo lo lote.

Palikuwapo Dameski Mkristo mmoja aliyeitwa Anania. Bwana alimwambia Anania katika maono kuondoka kwenda kwa nyumba ile ambamo Sauli alikuwamo, akamwekee mikoni ili Sauli apate kuona tena. Anania hakuelewa kwa nini Bwana alimtaka kwenda kumwona mtu huyu ambaye alikwisha kuwatesa Wakristo Yerusalemu. Lakini Mungu alimwambia kwamba alitaka kutumia Sauli katika kazi yake.

Anania alikwenda zake, akaingia mle nyumbani mwa Yuda ambamo Sauli alikuwamo. Alimwambia Sauli ya kwamba yeye ni Mkristo, na kwamba alikuja kumsaidia. Aliweka mikono yake juu ya kichwa cha Sauli, Sauli akapata kuona tena. Pia, Sauli alijazwa Roho Mtakatifu. Baadaye, Sauli alibatizwa, kisha akala chakula na akapata nguvu.

Baada ya kukaa na Wakristo wa Dameski kwa siku chache, Sauli alianza kuhubiri katika masinagogi,



akawaambia watu ya kwamba Kristo ndiye Mwana wa Mungu.

**KAZI YA KUFANYA**

Jaza nafasi katika sentensi hizo hapo chini kwa maneno yanayofaa.

1. Sauli aliwachukia ____________ ______________________________.

2. Sauli alifikiri kwamba alikuwa akimsaidia ________________kwa ____________________ Wakristo.

3. Sauli alipokuwa njiani kwenda Dameski ____________________.

4. Je! kulifanyika nini wakati Anania alipomwendea Sauli nyumbani mwa Yuda? __________ ______________________________ ______________________________ ______________________________ ______________________________

5. Sauli alitaka kufanya nini baada ya kugeuka kwa Mkristo? ________ ______________________________ ______________________________ ______________________________

Jibu sentensi zifuatazo kwa kuandika herufi "K" kando ya zile ambazo ni kweli, na kuandika herufi "M" (makosa) kando ya zile ambazo si kweli.

____ 1. Kwanza, sauli aliwachukia Wakristo.

____ 2. Kristo alisema na Sauli akiwa njiani kwenda Antiokia.

____ 3. Sauli aliacha dhambi na kumfuata Mwana wa Mungu.

____ 4. Anania hakwenda kumsaidia Sauli.

____ 5. Sauli alibatizwa.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe." Matendo 3:19a**

**Kutubu ni kusikitika kwa ajili ya dhambi zako. Inatupasa sisi sote kujaribu kutotenda dhambi. Lakini unapotenda dhambi, na kutubu, Mungu atakusamehe dhambi hizo zako na zitasahauliwa.**



**VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**

**MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU**

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Sura ya Pili

## KUMPA KRISTO NAFASI YA KWANZA

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 14:1-28**

Baada ya Paulo kuwa Mkristo, alitaka kumsimulia kila mtu habari za Kristo. Alihubiri Dameski kwa muda, lakini viongozi wengine wa kidini walikuwa wakipanga kumwua. Paulo alijua jambo hili. Alijua kwamba palikuwapo askari waliokuwa wakilinda mlango wa mji. Miji mingi nyakati zile ilikwa na kuta zilizozunguka na kuilinda kutokana na mashambulio. Marafiki za Paulo walitaka kumsaidia kwa hivyo walimshusha ukutani, wakimtelemsha katika kapu kubwa. Huu ulikuwa wakati wa usiku kwa hivyo hakuna mtu aliyeweza kuwaona. Kisha Paulo alirudi Yerusalemu. Baadaye akarejea kwao Tarso.

Kulikuwa na Wakristo katika Antiokia, waliokuja kuwaambia watu wa huko habari za Yesu. Kazi ya Bwana ilikuwa ikendelea, na Barnaba



aliyekuwa akihubiri huko alikata shauri kutaka msaada. Alimkumbuka Paulo na jinsi alivyompenda Bwana na kutaka kumtumikia. Alikwenda Tarso, akampata Paulo, wakaja naye Antiokia kumsaidia. Walifanya kazi

pamoja Antiokia kwa muda wa miaka miwili.

Siku moja, viongozi wa kanisa walikata shauri kwamba Paulo na Barnaba waondoke, waende mahali pengine kuwahubiria watu habari ya Kristo. Mji mmoja kati ya miji waliyokwenda uliitwa Ikonio. Walipofika katika mji huu, walikwenda sinagogini, wakawahubiria Wayahudi. Wayahudi wengi na Wayunani katika mji huu waliamini maneno ya Paulo na Barnaba waliosema, wakampokea Kristo kuwa Mwokozi wao. Baadhi ya Wayahudi wale walikasirika kwa sababu watu waliamini ya kwamba Yesu ndiye aliyekuwa Mwana wa Mungu. Wayahudi hawa waliwatupia Paulo na Barnaba mawe, wakawatoa nje ya mji huu wa Ikonio.

Paulo na Barnaba waliondoka Ikonio, wakaenda mahali palipoitwa Listra. Katika mji huo wa Listra, watu walidhania kwamba walikuwa miungu miwili; Herme na Zeu. Wakafanya sanamu ya miungu hawa walioabudu. Paulo alifanya mwujiza katika mji huu, kwa kumponya




mtu mmoja aliyekuwa kiwete tangu tumboni mwa mamaye. Mungu alikuwa akifanya kazi kwa Paulo, lakini watu hawakumjua Mungu. Walifikiri ya kwamba Paulo na Barnaba walikuwa miungu miwili, yaani Herme na Zeu, wakaanza kuwasujudia Paulo na Barnaba. Jambo hili liliwahuzunisha sana Paulo na Barnaba. Waliwaambia watu wale ya kwamba wao walikuwa tu wanadamu hali moja nao. Pia waliwaambia ya kwamba Mungu wa kweli ndiye aliyemponya kiwete yule, na kwamba Mungu ndiye aliyewaumba wote pamoja na vitu vingine vyote.

Wayahudi wengine kutoka Ikonio walikuja Listra wakiwatafuta Paulo na Barnaba. Waliwaambia watu ya kwamba Paulo na Barnaba walistahili kupigwa kwa mawe na kufukuzwa kutoka mjini. Walimpiga Paulo kwa mawe, wakamtoa nje ya mji wakidhania kuwa amekwisha kufa. Paulo aliumizwa vibaya sana lakini alisimama akaingia ndani ya mji, akakutana na Barnaba.

Paulo na Barnaba waliondoka Listra, wakaenda Derbe, mji uliokuwa karibu na Listra. Waliwahubiria watu huko kwamba Mungu alikwisha kumtuma Mwanawe ulimwenguni kufa kwa ajili ya dhambi za watu. Watu wengi waliamini wakaanza kumpenda Mungu wa kweli, na wakamwamini Kristo pia. Baada ya kuhubiri Derbe, Paulo na Barnaba walirudi Ikonio na Listra kuona jinsi waamini wapya katika miji hiyo walikuwa wakiendelea.

Walikuwa mashujaa sana kurudi katika miji ambako walikwisha kupigwa kwa mawe.

Hatimaye walirudi Antiokia kwa makanisa yale mawili huko. Washiriki wa makanisa yale walipendezwa kusikia mambo ambayo wamisheni hawa walipata kuyaona. Walimsifu Mungu kwa kufanya kazi yake kwao.

**KAZI YA KUFANYA**

Soma sentensi zifuatazo, kisha uweke alama hii ( X ) kando ya jibu sawa la kila sentensi.

1. Barnaba alimwuliza Paulo kuja kufanya kazi naye
( ) Yerusalemu ( ) Antiokia.

2. Paulo na Barnaba waliingia wapi walipofika Ikonio?
( ) sokoni ( ) sinagogini.

3. Ni nani waliompokea Kristo kama Mwokozi wao?
( ) Warumi ( ) Wayahudi wengi na Wayunani.

4. Kiwete yule katika Listra aliponywa kwa sababu alikuwa na
( ) imani ( ) pesa.

5. Watu wa Listra walifikiri Paulo na Barnaba walikuwa
( ) miungu ( ) malaika.

6. Wakati Paulo na Barnaba waliporudi Antiokia,
( ) walijisifu wenyewe
( ) walimsifu Mungu.

Jaza nafasi katika sentensi zifuatazo.

1. Marafiki za Paulo walimweka ndani ya ____________ wakamtelemsha ukutani ili apate kutoroka Dameski.

2. Paulo alirudi ____________ ____________ alipotoka Dameski.

3. Mjini kwao Paulo uliitwa ______ ____________.

4. Paulo alitaka kushiriki neno la ____________ na wengine.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu." Wakolosai 1:10**

Katika kifungu hiki, neno "mwenende" maana yake ni "kuishi". "Mkizaa matunda" maana yake kutenda mambo yanayompendeza Mungu. Inatupasa daima kutaka kumpendeza Mungu, tena inatupasa kujifunza mengi juu ya Mungu ambaye ni Baba yetu wa Mbinguni.

____ 4. Sila alifuatana na Paulo katika safari yake ya pili ya umisheni.

____ 5. Paulo na Sila waliabiri kwa mashua kwenda na miji ambao Paulo alikuwa bado hajapata kutembelea.

Piga mstari chini ya neno au maneno ya kweli katika sentensi zifuatazo:

1. (Siku moja) (Usiku) Paulo aliona maono, na katika maono hayo alimwona mtu aliyemwambia avuke aende Makendonia.

2. Watu (watatu) (wanne) walikwenda pamoja na Paulo Makedonia.

3. (Petro) (Mtabibu Luka) alikwenda pamoja na Paulo.

4. Wayahudi wa Filipi waliabudu (ndani ya sinagogi) (kando ya mto).

5. (Lidia) (Mariamu) alikuwa mmojawapo wa wanawake wale walioabudu kando ya mto.

6. (Watawala) (mlinzi wa gereza) alimwamini Bwana Yesu, akawa Mkristo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Nitamwimbia Bwana maadamu ninaishi; nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai."** **Zaburi 104:33**



# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Sura ya Tatu

## KUIMBA GEREZANI

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 16

Bwana alimgeuza Sauli kuacha hali ya kuwatesa Wakristo na kuwa mhubiri. Muda mfupi tu baadaye, Luka ambaye aliandika kitabu cha Matendo, alimwita Sauli kwa jina lingine. Alimwita Paulo.

Paulo alitaka kurejea katika mahali ambako yeye na Barnaba walikwisha kutembelea wakati wa safari yake ya kwanza ya umisheni. Alitaka kuona jinsi makanisa mapya waliyoyaanzaisha huko yalivyokuwa yakiendelea. Mtu mmoja, aitwaye Sila, alikwenda pamoja na Paulo katika safari hii. Katika safari ya kwanza, Paulo na Barnaba waliabiri kwa mashua kutoka Antiokia, lakini katika safari hii, Paulo na Sila walitembea kwa miguu kwenda Derbe na Listra, na kwa miji mingine ambako walikwisha kuanzisha makanisa mapya.

Katika Listra, Paulo alikutana na kijana mmoja aliyeitwa Timotheo. Kijana huyu alikuwa akimwabudu Mungu wa kweli maishani mwake. Mama yake na nyanya yake walikuwa wamemfundisha habari za Mungu wa kweli. Timotheo alipowasikia Paulo na Sila wakihubiri habari za Kristo, Mwana wa Mungu, aliamini mahubiri yao kuwa ni ya kweli, akawa Mkristo. Paulo na Sila walimpenda Timotheo, na walijua kwamba angeweza kuwa msaada kwao, kwa hivyo walimtaka afuatane nao.

Walitembelea mahali pengi ambapo Paulo alikuwa bado hajapata kutembelea mbeleni. Troa palikuwa mahali papya kwa Paulo. Hata siku moja usiku, wakati Paulo alipokuwa akikaa huko, aliona maono. Katika maono hayo alimwona mtu aliyemwambia, "Vuka, uje Makedonia utusaidie." (Matendo 16:9) Paulo alijua mara moja kwamba hilo ndilo

jambo ambalo Mungu alimtaka kufanya, kwa hivyo waliondoka mara moja Troa, wakaenda Makedonia. Mtu mmoja aitwaye Luka (daktari) pia alikuwapo pamoja nao.

Waliabiri kwa mashua kutoka Troa, wakafika Neapoli. (Tazama ramani katika Somo la Kwanza) Kisha wakatembea kwa miguu mpaka Filipi ambapo ndio uliokuwa mji mkuu wa sehemu ile. Watu wengi waliokaa pale walikuwa Warumi. Wayahudi walikuwa wachache sana pale, tena hapakuwapo sinagogi. Hata siku ya sabato, Paulo na wenzake walitaka kumwabudu Bwana. Waliambiwa ya kwamba kulikuwa na watu fulani waliofanya maombi kando ya mto. Paulo na wenzake walikwenda mtoni wakakuta kundi la wanawake pale wakiomba na kumsujudia Mungu. Waliketi chini, wakasema na wanawake wale juu ya Kristo, Mwana wa Mungu.



Wanawake wale walikwisha kusoma Maandiko ya Agano la Kale na walijua ya kuwa manabii walisema zamani kwamba Mwokozi angekuja siku moja. Baada ya kuwasikia Paulo na Sila wakiwaambia habari za Yesu, waliamini maneno yao.

Mmojawapo wa wanawake wale aliitwa Lidia. Alimpokea Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wake na akabatizwa. Aliwakaribisha Paulo na wenzake nyumbani mwake wakati ule walipokuwa Filipi.

Katika mji huu wa Filipi, kulikuwa na kijakazi kimoja aliyewapatia bwana zake faida nyingi kwa kuagua. Hii maana yake kwamba huyu aliwafuata Paulo na Sila kila mahali walipokwenda mle mjini. Alipaza sauti yake, akisema, "Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kuwahubiria njia ya wokovu." Alifanya hivi kwa siku nyingi. Paulo alijua kwamba alikuwa na pepo mchafu, basi siku moja aligeuka akamwambia yule pepo mchafu, "Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu." Pepo yule mchafu alimtoka kijakazi yule, kisha kijakazi yule hakuweza tena kuagua.

Jambo hili liliwahuzunisha mabwana za kijakazi yule sana walipoona ya kuwa tumaini la faida yao ya pesa limewapotea. Waliwakamata Paulo na Sila wakawapeleka kwa watawala. Waliwaambia watawala hao ya kwamba Paulo na Sila walikuwa wakichafua mji wao. Watawala waliwavua Paulo na Sila nguo zao, wakaamuru wapigwe kwa bakora. Kisha, baada ya kuwapiga, waliwatupa gerezani, wakamwamuru mlinzi wa gereza kuwalinda sana. Mlinzi aliwaweka Paulo na Sila katika chumba cha ndani cha gereza, akawafunga miguu na mkatale.



Paulo na Sila walikuwa wamekwisha kuteswa kwa mateso mengi ambayo kwayo wangeweza kulia, lakini badala ya kulia, waliimba nyimbo za kumsifu Mungu. Walianza kuimba usiku wa manane. Wafungwa wengine waliwasikia wakiimba wakashangaa kwa nini walikuwa na furaha.

Katika wakati huu wa kuimba kwao, kulitokea mtetemeko mkuu na misingi ya gereza ikatikisika. Ilikuwa mtetemeko wa nchi. Ilifanya milango yote ya gereza kufunguka, na vifungo vilivyokuwa mikononi na miguuni mwa wafungwa vililegezwa. Mlinzi wa gereza alipoona milango ya gereza ikiwa imefunguka, alidhania ya kuwa wafungwa wote walikuwa wamekimbia, kwa hivyo alitaka kujiua yeye mwenyewe. Paulo alimwona, akapaza sauti yake kwa nguvu, akamwambia, "Usijidhuru kwa maana sisi sote tupo hapa." (Matendo 16:28) Mlinzi aliingia ndani ya gereza ambako Paulo na Sila walikuwamo, akawaangukia miguuni mwao. Aliwauliza, "Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?" Walimwambia amwamini Bwana Yesu Kristo. Walimhubiria habari za Kristo, Mwana wa Mungu. Mlinzi aliamini akabatizwa. Kisha aliwaosha jeraha zao. Akawaandalia chakula, akawapa, wakala. Alikuwa sasa mtu aliyegeuzwa kabisa. Kabla ya kujua habari za Kristo, hakujali kama Paulo na Sila walikuwa na njaa au la, lakini sasa aliwajali.

Kulipopambazuka, Paulo na Sila waliambiwa kwenda zao, wakarudi nyumbani mwa Lidia, wakawapigia watu wa huko kwa heri kisha wakaondoka.

**KAZI YA KUFANYA**

Andika herufi hii "X" katika kila mstari ulio kando ya maneno ya kweli.

____ 1. Barnaba alifuatana na Paulo katika safari yake ya pili ya umisheni.

____ 2. Timotheo alikuwa kijana aliyemwamini Mungu.

____ 3. Paulo hakumchukua Timotheo.




Ki. ____________

Kifungu hiki kiandikwa na Yohana ambaye alikuwa pamoja na Yesu wakati Yesu aliposema maneno haya. Yesu alikuwa akizungumza na watu. Aliwaambia ya kwamba kama wangeshika maneno haya ya upendo mkuu wa Mungu katika akili zao na kuyaamini, na pia kumwamini Mungu, watakaa katika roho milele.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani." Yohana 5:24**

**VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**

**MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU**

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

**Sura ya Nne**

## PAULO AHUBIRI ATHENE

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 17:16-34

Katika somo hili tunamwona Paulo akiwa katika Athene, Uyunani. Anawatazamia Sila na Timotheo kuwasili. Na katika kuwangojea kuwasili, anazunguka huku na huko mle mjini. Paulo anachukizwa sana anapowaona watu wakiabudu sanamu au miungu wa uwongo. Alihuzunika sana ya kwamba watu wale hawakumjua Kristo kama Mwokozi wao. Aliingia ndani ya sinagogi ambayo Wayahudi waliabudia, akazungumza nao. Aliwakuta watu wengi sana sokoni kwa sababu watu wale walikwenda huko kuuza na kununua vitu. Pia, wanaume wengi walikwenda sokoni kuzungumza na kuonyesha jinsi walivyokuwa na maarifa mengi. Wayunani walikuwa watu waliojivunia maarifa yao, na sikuzote walikuwa na tamaa ya kujifunza mawazo mapya.



Baadhi ya watu wenye ujuzi walifikiri ya kwamba Paulo alikuwa akifundihsa juu ya Mungu mgeni. Walimwambia Paulo kupanda juu ya mahali palipoitwa Areopago na kuwahubiria habari za Mungu huyo mgeni kwao. Paulo alipanda juu ya Areopago, akasimama katikati, na

watu wale wakaketi juu ya mawe. Paulo aliwaambia, "Enyi watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini." (Matendo 17:22) Aliwaambia kwamba wakati alipokuwa akizunguka huku na huko, aliona madhababu iliyoandikwa maneno haya, "Kwa Mungu asiyejulikana." Kisha Paulo aliwaambia ya kwamba angewahubiria habari za Mungu huyo ambaye hawakumjua.

Paulo aliwaambia watu wale ya kwamba Mungu wa kweli ndiye aliyeumba ulimwengu na vitu vyote vilivyomo ndani. Yeye ndiye Bwana wa mbingu na nchi, na hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono. Paulo aliwaambia kwamba Mungu hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho chote. Mungu ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote.

Paulo alijaribu kuwafundisha watu hawa wa Athene ya kwamba Mungu ndiye aliyewaumba. Alitaka wafahamu ya kuwa miungu hawa waliotengenezwa kwa fedha, dhahabu au kwa kuchonga jiwe kwa mikono ya wanadamu havingeweza kuumba ulimwenguni kama huu ambao Mungu wa kweli alifanya.

Watu wale walikuwa wametenda dhambi na ilikuwa lazima watubu dhambi zao kwa Mungu kwa njia ya Kristo. Paulo alitaka wafahamu jambo hilo. Aliwaambia juu ya uzima wa milele pamoja na Mungu, kisha baadhi ya watu wale wakamdhihaki Paulo. Wengine walisema kwamba wangependa kusikia mengi juu ya mambo hayo.

Paulo alipomaliza kusema, alikata shauri kuondoka Athene. Watu wengine walimwamini Kristo wakaondoka naye.

Paulo alishiriki ujumbe wa Kristo na watu wale wa Athene. Watu wengi hawakuamini, lakini kulikuwa na wengine walioamini, na wangeshiriki ujumbe huo na wengine.

Sisi pia ni lazima tutambue kwamba inatupasa kushiriki Kristo na watu wengine. Ikiwa unamjua mtu ye yote ambaye hajui habari za Kristo kama Mwokozi wake, msimulie habari ya Kristo. Ukifanya hivyo utakuwa ukishiriki habari za Yesu kama Paulo alivyofanya.

**KAZI YA KUFANYA**

Soma sentensi zifuatazo kisha uweke alama hii ( X ) katika kila mstari ulio kando ya sentensi ya kweli.

____ 1. Paulo aliudhika alipoona mji wote wa Athene ukijaa sanamu na miungu wa uongo.

____ 2. Paulo alizungumza na Wayahudi ndani ya jengo la sinagogi ambalo Wayahudi walijenga kama mahali pao pa kuabudia.

____ 3. Kila siku Paulo alizungumza habari za Yesu sokoni na wale aliokutana nao.

Je! ni maneno yapi mageni ambayo Paulo aliona madhabahu iliyokuwa pale mjini? Andika maneno hayo chini ya picha ya madhabahu.



______________________________

Soma katika Matendo 17:24-26 mambo ambayo Paulo aliwaambia watu wa Athene juu ya Mungu. Sasa chora mstari kutoka kwa kila sentensi hapo chini hadi kwa neno linaloikamilisha.

| | |
|---|---|
| Mungu aliumba | nchi |
| Mungu ni Bwana wa mbingu na | ulimwengu |
| Mungu hakai ndani ya | watu wote |
| Mungu hatumikiwi kwa | mikono ya wanadamu |
| Kutoka kwa mtu mmoja Mungu alifanya taifa la | hekalu |

Soma Matendo 17:32-34 uone jinsi watu mbalimbali walivyofikiria ujumbe wa Paulo. Chini ya kila picha andika namba ya kifungu cha Biblia kinachoeleza habari yake.




Ki. ____________




Ki. ____________



# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

**Sura ya Tano**

## USIOGOPE

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 18:1-22**

Je! umepata kushona hema? Ushonaji hema ulikuwa kazi nzuri sana siku zile za Paulo. Paulo alipokuwa kijana mdogo alifundishwa kazi hiyo ya kushona hema. Na alipokua, akawa mtu mzima, alifurahi kujua kazi hii kwa sababu ilimsaidia sana kupata maishilio wakati alipokuwa akienda huko na huko akiwahubiria watu habari za Kristo, Mwana wa Mungu.

Je! umepata kuogopa? Paulo aliogopa wakati alipokuwa Korintho. Katika somo hili tutasoma jinsi Paulo alivyoshinda woga wake.

Paulo alipoondoka Athene alikwenda Korintho. Alikuwa na marafiki zake huko Korintho, nao walikuwa Akila na Prisila. Watu hawa walikuwa washonaji hema kama Paulo, na Paulo akakaa pamoja nao wakati alipokuwa Korintho. Alishirikiana nao kushona hema kwa sababu alihitaji pesa za kuishi. Hakutaka kuyaomba makanisa kumpatia pesa kwa sababu yeye mwenyewe angeweza kujipatia pesa kwa kazi hii.

Siku ya sabato Wayahudi wote walikwenda sinagogini kumwabudu



Mungu. Paulo pia alikwenda sinagogini. Alijua Wayahudi hawa hawakujua habari za Kristo kama Mwana wa Mungu aliyeahidiwa kuja, kwa hivyo alikuwa na tamaa ya kuwaambia habari hizo. Paulo aliwaza hasa moyoni mwake ya kwamba Wayahudi hawa walipaswa kuokolewa.

Sila na Timotheo pia walikuwa wamekwisha kuwasili Korintho, na walimsaidia Paulo. Wayahudi hawakupokea ujumbe wa Mungu kuwa ni wa kweli. Hawakufikiri ya kwamba Yesu wa Nazareti alikuwa Mwokozi aliyeahidiwa kuja. Paulo aliwaambia kwamba alikwisha kujaribu kuwasaidia wapate wokovu lakini wao walikuwa wajeuri kwake. Aliwaambia hangewahubiria tena sinagogini. Alisema ya kwamba angewapelekea watu wa Mataifa ujumbe wake.

Paulo aliingia katika nyumba moja iliyokuwa imepakana na sinagogi kufanya mikutano yake ndani. Nyumba hiyo ilikuwa ya mtu mmoja aliyeitwa Tito Yusto, na alifurahi sana kumpokea Paulo kuhubiri nyumbani mwake. Watu walianza kuamini ujumbe huu wa Kristo. Krispo, ambaye alikuwa mkuu wa sinagogi, alimwamini Bwana pamoja na jamaa yake yote. Wakorintho wengi walimsikiliza Paulo akifundisha, wakaamini, kisha wakabatizwa.

Wayahudi wasioamini walimkasirikia sana Paulo, wakaanza kumtisha. Paulo aliwaogopa, ingawa alikuwa shujaa. Mungu alijua woga uliokuwa moyoni mwa Paulo. Siku moja usiku, "Bwana akamwambia Paulo kwa maono usiku, Usiogope, bali nena, wala usinyamaze." (Matendo 18:9) Mungu alimwahidi Paulo ya kwamba angekuwa pamoja naye, na kwamba hakuna mtu ye yote ambaye angemshambulia.

Paulo alikuwa na imani katika Mungu na alijua kwamba Mungu angetimiza ahadi hiyo yake. Alikaa Korintho akifundisha Neno la Mungu kati ya watu kwa muda wa mwaka mmoja na nusu.

Sisi sote tuna woga. Je! unaogopa kuwafanya wengine kujua kwamba unampenda Bwana Yesu? Kumbuka Bwana anasema, "Nitakusaidia."

## KAZI YA KUFANYA

Chora mstari chini ya jibu sawa la kila swali.

1. Je! Paulo alikaa pamoja na mume na mke yupi katika Korintho?

Anania na Safira

Akila na Prisila

2. Je! walifanya kazi gani?

Kushona hema

Kuvua samaki

Kulima

3. Paulo alikuwa amfundishwa kazi. Je! kazi hiyo ilikuwa nini?

Kulima

Kufuga kondoo

Kushona hema

4. Je! Paulo alihubiri wapi siku ya Sabato?

Sokoni

Sinagogi

Njiani

5. Aliwahubiria watu gani?

Warumi

Watu wa Athene

Wayahudi

Kata maneno ambayo si kweli katika sentensi zifuatazo.

1. Wayahudi hawakuamini Injili ya Kristo, kwa hivyo, Paulo aliwaambia ya kuwa angekwenda kuwahubiria (Warumi) (Mataifa).

2. Paulo aliingia katika nyumba ya mtu mmoja aliyeitwa (Yusto) (Akila). Mtu huyu alikuwa wa Mataifa na alimwabudu Mungu. Nyumba yake ilipakana na (soko) (sinagogi).

3. Krispo, (kuhani) (mkuu) wa sinagogi, pamoja na jamaa yake (hawakumwamini) (walimwamini) Kristo.

4. Watu wengine (wengi) (wachache) katika Korintho pia walimwamini Kristo.

5. Mungu alisema na Paulo katika maono (akamwambia alikuwa hatarini kwa hiyo ilimpasa kuondoka) (akamwambia akae na kuwahubiria watu, wala asiogope).

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa maana mimi, Bwana, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; mimi nitakusaidia."
Isaya 41:13

Ikiwa wakati wo wote unaweza kutembea katika mahali penye giza, labda unaweza kuogopa. Lakini ikiwa kuna mtu anayekushika mkono wakati unapotembea mahali hapo penye giza, hutakuwa na woga. Mungu atakushika mkono katika maisha yako yote, kwa hivyo anakwambia, "Usiogope."



# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Sura ya Sita

## KUPENDEZA MUNGU BADALA YA MWANADAMU

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 19:23-41**

Je! ni nani anayetaka maadui? Watu wengi hawataki maadui. Ni jambo la kawaida kwa mtu kutaka kuwa na marafiki na kutaka watu kumpenda.

Mtume Paulo alitambua ya kwamba kadiri aliyompendeza Kristo ndivyo alizidi kuwa na maadui



wengi. Katika somo hili tutaona kuwa ni mambo gani yaliyompata katika safari yake ya tatu ya umisheni.

Paulo alirudi Efeso akahubiri sinagogini kwa muda wa miezi mitatu. Wayahudi wengine ambao hawakumwamini Kristo, walianza kusema maneno maovu juu ya Neno lile ambalo Paulo alihubiri. Paulo hakurudi tena sinagogini. Aliwachukua wanafunzi wake wakaenda katika darasa la mtu mmoja aliyeitwa Tirano. Alihubiri hapa kwa miaka miwili hata wakazi wote wa Asia wakasikia neno la Bwana, Wayahudi na Wayunani. (Matendo 19:10)

Katika Efeso watu waliabudu mungu mke aliyeitwa Artemi. Watu walinunua sanamu ndogo za mungu huyu kuweka nyumbani mwao. Hata wakati wa kusafiri walichukua sanamu hizo na kusafiri nazo

wakifikiri kwamba zingeweza. Sanamu kubwa ya Artemi ilikuwa hekaluni. Pia watu walinunua vihekalu vya sanamu hiyo.

Demetrio alikuwa mfua fedha, na alifanya vihekalu vya fedha vya Artemi. Alikuwa akipata faida kubwa kwa kuuza vihekalu hivyo vya dhahabu. Mafundi wengine walikuwa wakifanya sanamu na vihekalu kwa miti, jiwe, au chuma na walikuwa wakipata pesa nyingi sana. Demetrio alitambua kuwa watu walikuwa hawanunui sanamu tena. Alifanya mkutano na kuwaita mafundi wengine, akawaambia ya kwamba watu walikuwa wakimwamini Kristo kwa sababu ya mahubiri ya Paulo. Aliwakumbusha ya kwamba Paulo alikuwa amesema ati miungu waliochongwa na wanadamu si miungu wa kweli. Alizidi kuwaambia ya kwamba hawangekabiliwa na hatari ya kupoteza biashara hiyo yao peke yake bali mungu huyo mke (Artemi) angehesabiwa kuwa si kitu; na watu wangeidharau.

Mafundi wale waliposikia hayo, walikasirika sana wakapaaza sauti zao wakisema, "Artemi wa Efeso ni mkuu." Mji wote ulijaa ghasia. Mara kwa mara watu wachache wanapoanzisha ghasia njiani, watu wengine huwafuata. Hivyo ndivyo watu wengine walivyojiunga katika ghasia zile na makelele; wakisema, "Artemi wa Efeso ni mkuu." Wengine kati yao hata hawakujua sababu ya kukusanyika kwao pamoja. Walikuwa na wasiwasi mkubwa sana wakawaburuta wanafunzi wawili wa Paulo wakawaweka uwanjani mbele ya watu. Biblia yote haitambii sababu ya wao kufanya hivyo, wala haitaji kama watu hawa walidhuriwa katika njia yo yote.

Paulo alisikia mambo haya, alitaka kwenda huko uwanjani kuingia kati ya watu, lakini marafiki zake wengine walimshawishi asiingie. Walimzuia akiingia ghasia zingeongezeka. Mchafuko huu uliendelea kwa saa nyingi. Hatimaye karani wa mji aliwatuliza watu. Baada ya kelele kwisha, Paulo aliwaita wanafunzi wake, na baada ya kuagana nao, aliondoka kwenda Makedonia.

Vijana, vile Mungu alivyomlinda na kumwongoza Paulo katika mji wa Efeso, vivyo hivyo atawaongoza ninyi pia. Ukichagua kumpendeza Kristo kuliko kumpendeza mwanadamu, Mungu atakuwa nawe na atakusaidia.

**KAZI YA KUFANYA**

Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo.

1. Katika somo hili tunamwona Paulo katika mji wa ____________.

2. Kwanza, Paulo alihubiri katika ____________________________.

3. Paulo aliondoka akaenda akahubiri katika ______________.

4. Demetrio aliyekuwa mfua fedha maarufu katika Efeso alitengeneza ______________________________ na kujipatia faida pesa nyingi.

Picha hiyo hapo chini inaonyesha hekalu, pesa, na mikono. Chora mstari kutoka kwa kila swali hadi kwa mojawapo ya vitu hivyo pichani ambacho ndicho jibu la swali hilo.



1. Je! ni kitu kipi katika picha kinachoonyesha kwamba wafua fedha walipata kwa kufanya sanamu?



2. Je! Paulo alisema kwamba Mungu hawezi kufanywa kwa nini?



3. Je! watu wa Efeso wangehesabu nini kuwa si kitu kama wangeendelea kumsikiliza Paulo?

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Nimemweka Bwana mbele yangu daima, kwa kuwa yuko kuumeni kwangu, sitaondoshwa."**

**Zaburi 16:8**

Ikiwa unajaribiwa kutenda jambo lisilo haki, hutakubali jaribu hilo kama Bwana yupo mbele yako. Hutaweza kuondolewa katika kutenda jambo lililo haki machoni pake.



**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, "Mimi hapa, nitume mimi." Isaya 6:8**

Bwana wetu anawatafuta Wakristo watakaojitoa kwake. Anataka waamini watakaokwenda mahali po pote wakati wo wote kuwahubiria wengine Habari Njema ya wokovu.



# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA    KITABU CHA TATU

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Sura ya Saba

## PAULO AENDA YERUSALEMU

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 20:13-38; 21:1-19**

Je! wewe ni mtu anayefanya mambo unayofikiria kuwa haki ingawa marafiki zako wanajaribu kukubadili nia? Kwa mfano, umekuwa shuleni mchana wote na umepewa masomo ambayo ni lazima kujifunza kabla ya keshoe. Kisha marafiki zako wanakuja na kukuambia, "Njoo tucheze mpira kwa muda. Itakuwa vizuri kwako kufanya mazoezi baada ya kuwa shuleni mchana wote." Wewe mwenyewe unajua wazi ya kwamba mazoezi yatakuwa mazuri kwako. Pia unajua kwamba usipoanza mara moja kujifunza, hutaweza kumaliza masomo hayo. Je! utafanya nini?

Kwa mfano mwingine unafanya kazi ya kuuza dukani. Je! utatoa udhuru mbalimbali kwa kutoweza kwenda kazini? Labda una homa kidogo tu na unasema, "Nitakaa nyumbani." Mwenye duka anakutegemea wewe kuwa kazini. Je! utafanya nini? Tena kwa mfano, una Biblia yako na gitaa. Je! utakuwa na tamaa ya kuwaonyesha marafiki zako Biblia au gitaa? Unafikiria marafiki zako watakudhihaki kwa sababu unajivunia Biblia yako? Kuwa na gitaa si vibaya, lakini Bwana wetu anawataka watu ambao watatenda mema na ambao hawataona aibu kutenda haki. Wakati mwingine marafiki zetu wana usio mzuri kwetu. Katika hali kama hiyo inatupasa kuwa imara na kufanya mambo tunayofikiri kuwa haki.

Katika somo hili juu ya Paulo, tunaona ya kwamba Paulo alikataa kushawishiwa kutoamini mambo ambayo Bwana alimtaka kufanya. Paulo aliweka madhumuni yake mwenyewe. Je! umeweka madhumuni kwa maisha yako? Labda umekwisha kuweka

madhumuni au lengo la kutimiza wakati ujao wa mapumziko. Labda umekwisha kukata shauri kuwa mwuguzi, au mwalimu, au mhubiri, au daktari, au kufanya kazi yo yote.

Paulo alikuwa na madhumuni ya kwenda Yerusalemu kudhimisha sikukuu ya Pentekoste. Alikuwa katika safari yake ya tatu ya umisheni ambapo shida kubwa ilitokea kati yake na mafundi wa kufua fedha Efeso. Baada ya kuondoka Efeso alisafiri kwa miguu kupitia Makedonia mpaka Uyunani. Alikaa Uyunani kwa miezi mitatu kisha akapanga kuabiri kwa mashua (Merikebu) kwenda Shamu na hatimaye kurejea Yerusalemu. Alisikia ya kwamba Wayahudi wengine walikuwa wakipanga kumwua wakati wa kuingia mashuani kwenda Shamu, kwa hivyo aliamua kutembea kwa miguu kupitia tena Makedonia. Wakati alipofika Filipi aliingia mashuani, akaenda Troa. Luka na Timotheo walikutana naye Troa wakakaa pamoja kwa muda wa siku saba.

Katika mji huu wa Troa jambo fulani la kustaajabisha lilifanyika. Paulo alikuwa akiwahubiria watu katika chumba cha orofa. Katika chumba hicho palikuwa na kijana mmoja aliyekuwa ameketi dirishani. Alisikiliza mahubiri ya Paulo kwa muda mrefu, na akalala, akaanguka kutoka pale dirishani. Orofa hiyo ilikuwa ya tatu kwa hivyo watu walifikiri bila shaka kijana huyo alikufa. "Paulo akashuka, akamwangukia, akamkumbatia, akasema, Msifanye ghasia, maana uzima wake ungalimo ndani yake." (Matendo 20:10) Watu walimwondoa kijana huyu akiwa mzima hasa.

Paulo aliendelea na safari yake. Katika Tiro Wakristo walimwonya asiende Yerusalemu kwa sababu maisha yake yangekuwa hatarini. Paulo aliwaeleza ya kuwa aliwaza moyoni mwake kwamba Bwana alimtaka kwenda Yerusalemu. Wakati wa Paulo wa kuondoka Tiro ulipofika, Wakristo wote waliondoka wakamsindikiza mpaka mashuani. Na kabla ya kwenda, wote walipiga magoti pwani, wakaomba.



Baada ya kuabiri kwa muda tulisimama Kaisaria. Katika mji huu Paulo na marafiki zake walikaa nyumbani mwa Filipo kwa muda. Na hapa tena Paulo alionywa asiende Yerusalemu kwa sababu kama angeenda atafungwa gerezani. Lakini Paulo aliwaambia marafiki zake hawa ya kwamba yeye alikuwa tayari hata kuuawa kwa ajili ya Bwana, licha ya kufungwa. Marafiki zake wakasema, "Mapenzi ya Bwana na yatendeke." (Matendo 21:14b)

Paulo alijua ya kwamba alikuwa anakabili hatari kwa kwenda Yerusalemu, lakini aliona ni heri kwenda huko kwa sababu ilikuwa mapenzi ya Mungu kwake kwenda Yerusalemu. Marafiki zake hawakutaka ateseke, na hata yeye mwenyewe hakutaka kuteseka, lakini alitaka kumtii Bwana. Madhumuni aliyokuwa ameweka yalikuwa kwenda Yerusalemu, na aliwaza moyoni mwake ya kwamba kwa kutimiza madhumuni hayo yake pia ingekuwa kufanya mambo ambayo Mungu alimtaka kufanya.

Je! madhumuni yako ni nini? Je! utasema na Mungu sikuzote kuhusu jambo unalotaka kufanya maishani mwako? Je! utafanya jambo unalofikiria kuwa haki na jema na ambalo ni mapenzi ya Mungu?

**KAZI YA KUFANYA**

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuandika majibu ya kweli katika nafasi zilizoachwa.

1. Paulo alikuwa amepanga kwenda Uyunani. Alibadilisha nia yake kwa sababu ________________

________________________________

________________________________.

2. Waamini wa Tiro walimwonya Paulo ya kwamba ________________

________________________________

________________________________.

3. Wakati wa Paulo kuondoka Tiro ulipofika, Wakristo wote walimsindi kiza mpaka________________.

4. Kabla Paulo kuondoka Tiro,

________________________________

pwani, wakaomba.

5. Katika Kaisari, Paulo na marafiki zake walikaa nyumbani mwa

________________________________.

Katika Kaisaria, marafiki za Paulo walimsihi asiende Yerusalemu. Lakini Paulo aliwaambia kwamba alikuwa tayari kuuawa kwa ajili ya Bwana. Marafiki zake hawakuweza kumbadili nia. Katika picha andika maneno ambayo walimwambia.

2. Paulo alisema ya kwamba yeye alikuwa

Mwafrika

Mtu mwema

Raia wa Rumi.

3. Paulo hakupigwa lakini

Aliwekwa gerezani

Alipewa kitanda laini

Aliambiwa kusoma sheria.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake."**

**Wafilipi 1:29**

Wakati Paulo alipoandika maneno haya kwa Wafilipi, alikuwa amekwisha kuteseka kwa ajili ya Kristo. Alisema, "Mmepewa," na kwake ilionekana kama baraka aliyopewa wakati alipoteseka kwa ajili ya Kristo.



# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU

## PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Sura ya Nane

## KUTESEKA KWA AJILI YA KRISTO

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 21:18 - 22:29**

Utakumbuka kwamba Paulo alionywa asiende Yerusalemu kwa sababu maisha yake yangekuwa hatarini huko. Paulo alikwenda Yerusalemu, na tutajifunza kwamba onyo hili lilikuwa zuri kwa sababu Paulo alikabiliwa kweli na hatari kubwa Yerusalemu.

Paulo aliwaeleza wazee wa Kikristo mambo yote ambayo Mungu aliyatenda kwa huduma yake. Wazee hao walikuwa na tamaa kwa Wakristo wengine Wayahudi kuelewa mambo hayo na kumwamini Paulo; lakini wengine kati ya Wayahudi hao walikuwa wamekwisha kumsikia Paulo akihubiri mambo kinyume cha sheria za Wayahudi kwa hivyo hawakumwamini. Paulo alikwenda pamoja na Wayahudi wanne na wakaingia hekaluni kujitakasa kama wazee wale walivyodokeza. Wote walioga, wakanyoa vichwa vyao, Kufanya hivi kungewadhibitishia Wakristo Wayahudi ya kwamba Paulo aliheshimu sheria za Kiyahudi.

Wayahudi wengine wasioamini ambao walitoka Asia walimwona Paulo ndani ya hekalu. Pia walimwona siku moja na marafiki wake wa Mataifa wa Efeso wakitembea. Waliamua kuwataharikisha Wayahudi wa Yerusalemu juu yake wakawaambia ya kwamba Paulo aliwaingiza marafiki zake wa Mataifa hekaluni. Wayahudi walifikiri kwamba wao ndio waliokuwa wateule wa Mungu, na kwamba Mataifa hawakupaswa kuingia hekaluni. Wayahudi wale walisema ati Paulo alikuwa akifundisha mambo kinyume cha Wayahudi na kwamba pia amekuwa akifundisha kinyume cha sheria za Kiyahudi na kinyume cha hekalu lao.



Wayahudi wa Yerusalemu hawakungojea kupata ukweli juu ya maneno hayo. Walimkamata Paulo, wakamburuta na kumtoa nje ya hekalu, wakafunga milango. Walikuwa na nia ya kumwua, lakini hawakutaka kumwua ndani ya hekalu.

Walianza kumpiga Paulo na kupiga makelele mengi sana hata habari zikawafikia askari ambao walikuja, wakamchukua Paulo, wakaenda naye ngomeni walikokaa.

Walipokuwa wakipanda ngazi kuingia ngomeni, Paulo alimwuliza jemadari kama angemruhusu kusema na watu, na jemadari akamruhusu. Paulo alisema na jemadari huyo kwa lugha ya Kiyunani, lakini akasema na Wayahudi kwa lugha ya Kiyahudi. Aliwaambia jinsi alivyowatesa Wakristo. Aliwaambia jinsi alivyogeuzwa na kumwamini Kristo, jinsi nuru ilimwangazia kote kote na kumpofusha macho na jinsi Anania alivyomwezesha kuona tena. Wayahudi walikuwa kimya na kumsikiliza Paulo akiwaambia mambo haya. Kisha Paulo aliwaambia maono ambapo katika maono hayo Bwana alimwambia, "Enenda zako; kwa kuwa mimi nitakutuma uende mbali kwa watu wa Mataifa." Neno hilo Mataifa liliwakasirisha Wayahudi wale, wakataka Paulo auawe.

Jemadari hakuweza kuelewa mambo ambayo watu walikuwa wakisema .wala hakuelewa maneno Paulo aliyoyasema. Hakujua kama



watu walimkasirikia sana Paulo na kutaka auawe. Alifikiri tu ya kwamba Paulo alikuwa amefanya jambo fulani baya sana ambalo liliwakasirisha watu wale. Aliamuru kwamba Paulo afungwe kwa kamba ili apate kupigwa. Jemadari huyu alifikiri ati kama Paulo angepigwa, angeweza kutoa sababu ya jambo lile alilofanya ambalo liliwakasirisha sana watu. Lakini Paulo alimwambia (jemadari huyu) ya kwamba yeye alikuwa raia wa Rumi. Kulingana na sheria za Kirumi, hakuna raia ye yote wa rumi ambaye angeweza kufungwa wala kuadhibiwa kwa njia yo yote mpaka anapopatikana na hatia. Kwa hivyo Paulo aliepuka kupigwa, lakini aliwekwa gerezani mpaka jemadari angeweza kupata habari nyingi juu yake. Tena, alikuwa bila hatari huko gerezani.

## KAZI YA KUFANYA

Paulo aliingia hekaluni Yerusalemu. Alitaka kuwaonyesha Wayahudi kwamba alishika sheria za Mungu. Wakati Wayahudi wengine wasioamini walipomwona (Paulo) ndani ya hekalu, waliamua kuwataharukisha watu juu yake. Weka herufi hii "X" kando ya mambo manne ambayo Wayahudi walishtaki Paulo kufanya.

____Kufundisha mambo kinyume cha watu.

____Kufundisha mambo yanayopinga dhambi.

____Kufundisha mambo kinyume cha sheria.

____Kufundisha mambo kinyume cha hekalu.

____Kumwingiza Myunani ndani ya hekalu lao takatifu.

Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo kwa majibu ya kweli.

1. Paulo aliongea lugha gani na jemadari? ________________

2. Paulo aliongea lugha gani na Wayahudi? ________________

3. Ni jina lipi Paulo alilolitaja ambalo liliwakasirisha sana Wayahudi? ________________

Chora mviringo kwa maneno ya kweli katika sentensi zifuatazo.

1. Jemadari aliwaamuru askari zake

**Kumlisha**

**Kupigana**

**Kumpiga Paulo.**

Klaudio Lisia kwa liwali mtukufu ________, __________! Mtu huyu alikamwatwa na W__________, wakawa karibu kumwua, ndipo nikaenda pamoja na ________cha askari nikamwokoa, nilipopata ______ ya kuwa yeye ni M________. Nami nikitaka kulijua lile neno waliom_________, nikamtelemsha nikamweka mbele ya baraza; nikaona kwamba ameshitakiwa kwa ajili ya maswali ya _______ yao, wala hakushtakiwa n__ l_ l___ la kustahili kuuawa wala kufungwa. Hata nilipopewa habari kwamba patakuwa na v________ juu ya mtu huyu, mara nikampeleka ________, nikawaagiza na wale waliom________, wanene habari zake mbele yako. Wasalamu.

Matendo 23:26-30



# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Sura ya Tisa

## MUNGU AMLINDA PAULO

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 22:30; 23:1-35**

Katika somo lililopita juu ya Paulo, utakumbuka kwamba Wayahudi wa Yerusalemu walimkasirikia sana. Katika somo hili utaona ya kuwa wangali wanamkasirikia, hasa anapotolewa ngomeni na kuletwa mbele ya baraza. Baraza hili ni kama korti ya sasa, na kuhani mkuu ndiye aliyesimamia baraza hilo badala ya jaji. Inaonekana kwamba Paulo alitoka katika shida moja na kuingia katika nyingine. Kwanza aliposimama kusema, alisema maneno yaliyomkasirisha kuhani mkuu, na kuhani huyo mkuu akamwamuru mtu aliyekuwa akisimama karibu naye kumpiga kinywa chake. Paulo alijua kwamba jambo hili lilikuwa kinyume cha sheria kwa mtu kumpiga. Alimwambia kuhani mkuu hivyo na kumwita kwa jina la ukuta uliopakwa chokaa. Je! unajua maana ya jina hilo? Maana yake ni kwamba kuhani



huyo mkuu alikuwa akijifanya tu, wala hakutii kweli sheria za Mungu, lakini alivunja sheria moja wakati alipomwamuru mtu aliyesimama karibu na Paulo kumpiga kinywa chake.

Paulo alikuwa mwerevu sana. Alijua ya kwamba sasa hangehukumiwa kulingana na sheria, kwa hivyo alifikiria njia ya kushinda kesi yake. Yeye alikuwa Farisayo, na sehemu ya baraza hili lilikuwa Mafarisayo. Alikata shauri kuleta mashindano baina ya Mafarisayo na Masadukayo. Masadukayo hawakuamini kwamba kuna ufufuo wa wafu wala malaika wala roho.

Mafarisayo waliamini mambo hayo yote. Paulo alipaza sauti yake katika ile baraza, "Mimi ni Farisayo; mimi ninahukumiwa kwa ajili ya tumaini ya ufufuo." Mafarisayo wote waliposikia hayo, wote walikuwa upande wa Paulo, wakasema hawakuona uovu wo wote kwake.

Jambo hili liliwakasirisha sana Masadukayo na ugomvi mkubwa ukatokea. Jemadari aliogopa ya kwamba pengine Paulo angeraruliwa nao, kwa hivyo aliwaamuru askari kumchukua Paulo na kumrudisha ngomeni.

Labda Paulo alikufa moyo. "Usiku ule Bwana akasimama karibu naye, akasema, Uwe na moyo mkuu; kwa sababu, kama ulivyonishuhudia habari zangu Yerusalemu, imekupasa kunishuhudia vivyo hivyo Rumi nako." (Matendo 23:11)

Palikuwapo Wayahudi arobaini waliokusudia kumwua Paulo. Kesho yake walifanya mpango wakajifunga kwa kiapo kwamba hawangekula wala kunywa kitu cho chote mpaka wamwue Paulo. Walipanga mpango na mkuu wa makuhani na wazee ya kwamba waamuru Paulo aletwe mbele ya baraza. Waliwaambia mkuu huyo wa makuhani na wazee ya kwamba wangemwua Paulo njiani kabla hajakaribia baraza.

Mtoto wa dada ya Paulo alisikia mipango hiyo yao, akaenda ngomeni akampasha Paulo habari. Paulo alimwita mmojawapo wa askari kumpeleka mtoto huyu kwa jemadari. Mtoto huyu alimwambia jemadari mambo aliyoyasikia kuhusu mipango ya watu wale ya kumwua Paulo. Jemadari alimwonya asimwambie mtu ye yote ya kwamba alimpasha habari hiyo.

Kisha jemadari alifanya mipango fulani ya siri. Aliamua kumwondoa Paulo Yerusalemu usiku ule. Paulo alikuwa chini ya mamlaka yake na hakutaka adhuriwe. Aliwaamuru askari walinzi mia mbili, askari wapanda farasi sabini na wenye mikuki mia mbili kumpeleka Paulo Kaisaria mbele ya Feliki Liwali. Pia alimpelekea Feliki barua ya kumjulisha juu ya mambo hayo.

Askari walinzi walimpeleka Paulo mpaka kwa Antipatri usiku ule kisha wakarudi ngomeni. Askari wale wapanda farasi ndio walimchukua Paulo na kuendelea na safari.

Walifika Kaisaria wakampa Feliki barua ile, wakamweka Paulo mbele yake. Paulo aliwekwa tena chini ya ulinzi akangojea mkuu wa makuhani na wazee wale kutoka Yerusalemu kuwasili Kaisaria.

**KAZI YA KUFANYA**

Katika baraza kulikuwa na makundi mawili, Mafarisayo na Masadukayo. Makundi haya yalitofutiana katika imani yao. Paulo alikuwa Farisayo. Baada ya muda usio mrefu, makundi haya mawili waliingia katika mabishano makali juu ya Paulo. Mafarisayo walisema, "Hatuoni uovu wo wote katika mtu huyu." Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo.

1. Jemadari aliogopa kwamba

Paulo angefanywaje? ____________

______________________________

2. Wakati Paulo alipokuwa ngomeni ni nani aliyemtia moyo usiku?

______________________________

______________________________

3. Wayahudi wale arobaini wenye hasira walipanga kufanya nini?

______________________________

______________________________

4. Ni nani aliyesikia mpango huo wao na kwenda kumwonya Paulo?

______________________________

______________________________

5. Jemadari aliamua kumpeleka Paulo Kaisaria. Je! alimpeleka kwa nini?

______________________________

______________________________

______________________________

Liwali Felik alitaka kujua habari ya mfungwa huyu mpya. Jemadari Lisia aliituma barua. Andika maneno kujaza nafasi zilizoachwa katika ukarasa ujao.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?**

**Waraka kwa Waebrania 13:6**

Paulo aliamini kweli ya kwamba Bwana alimsaidiaye wakati wo wote alipomhitaji. Ikiwa unaweza kuwa na imani ya namna hii, hutaogopa kwamwe.



# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU

## PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Sura ya Kumi

## KUMSHUHUDIA KRISTO

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 25:13-27; Matendo 26:1-32**

Inasemekana kwamba Paulo alikuwa mtu mdogo. Umekwisha kuwa pamoja naye katika safari nyingi na labda unaweza kuwa na mawazo yako mwenyewe juu yake. Labda alikuwa mdogo kimwili, lakini Je! unafikiri alikuwa mdogo katika ushujaa? Je! unafikiri alikuwa mdogo katika maarifa? Unafikiri alikuwa mdogo katika imani kwa Baba yake aliye mbinguni? La, hakuwa mdogo. Katika njia hizi na nyingine nyingi, Paulo alikuwa mkuu. Alikuwa mkuu katika upendo wake wa Kristo na katika tamaa yake ya kushiriki habari njema na wengine.

Paulo alitumia kila nafasi kumshuhudia Kristo. Kumshuhudia Kristo huwafadhaisha Wakristo wengine mpaka wanapoelewa hasa maana yake. Kushuhudia ni kushiriki habari njema, ukiwajulisha wengine



kwa Kristo anayewapenda na anayewataka kuwa na uzima wa milele. Kabla ya kuwashuhudia wengine, kwanza ni lazima kuwa na hakika juu ya jambo unaloamini. Hakikisha kwamba unamjua Yesu kama Mwokozi na Bwana wako. Kristo akiwa halisi kwako na kuwa karibu nawe, utajua mambo anayoweza kuwafanyia wengine.

Katika somo hili, Paulo anasimama mbele ya watu fulani muhimu. Anafurahi kujitetea mbele ya Mfalme Agripa kwa sababu mfalme huyu alikuwa Myahudi na alijua sheria za Kiyahudi kuanzia historia ya Agano la Kale. Bernike dadaye Agripa pia alikuwapo pamoja naye. Pia, Festo liwali alikuja tena kumsikia Paulo.

Festo liwali alikuwa amekwisha kumwambia mfalme Agripa habari za Paulo. Alikwisha kumpasa habari kwamba Paulo alitaka rufani kwa Kaisari. Alitaka sana kumsikia Paulo akisimulia habari zake tena ili angeweza kupata jambo la kumshtaki. Lakini hata hivyo, Festo hakuweza kufikiria wala kuona shtaka lo lote baya juu ya Paulo. Ilikuwa desturi kumpeleka mfungwa ye yote atakayepatikana na hatia mbaya sana kwa Kaisari, katika Rumi, lakini Paulo hakuwa na hatia yo yote wala hakuvunja sheria yo yote ya Kirumi.

Paulo alianza kusimulia habari zake kwa kueleza jinsi alivyowatesa Wakristo kabla hajawa Mkristo yeye mwenyewe. Kisha alisimulia juu ya ugeuzi wake katika njia ya kwenda Dameski. Je! unakumbuka mambo yaliyomfanyikia Paulo? Yasome tena. Pia, Paulo aliwaambia watu hawa muhimu ya kwamba Bwana alimwambia kuwahubiria Wayahudi na watu wa Mataifa. Alimtii Bwana akawahubiria Wayahudi habari za Kristo. Kisha alisafiri kwenda nchi za mbali na kuwaambia watu wa Mataifa habari za Kristo.

Wakati Paulo alipomaliza kusema, wakuu wale waliondoka mle chumbani kwenda kusemezana juu ya kesi ile. Hawakuona jambo lo lote baya ambalo Paulo alitenda lilimfanya kufungwa. Wote walikubaliana pamoja ya kwamba kama Paulo hangalikuwa ametaka rufani kwa Kaisari angefunguliwa, lakini rufani hii haingeweza kubadilishwa.

Paulo aliwaza moyoni mwake kwamba Mungu ndiye aliyemtaka kwenda Rumi. Na sasa alikuwa anakwenda huko ingawa alikuwa anakwenda kama mfungwa.

**KAZI YA KUFANYA**

**Mfalme Agripa na Bernike dada yake walikuja Kaisaria ambako mtume Paulo alikuwa mfungwa. Chora mviringo kwa herufi "K" iliyo kando ya sentensi ya kweli, na uchore mviringo kwa herufi "M" iliyo kando ya sentensi ambao si kweli.**

K M Mfalme Agripa na Bernike walikuja kumkaribisha Festo.

K M Festo Liwali alimwambia mfalme ya kwamba Paulo alikuwa na hatia.

K M Viongozi wa kiyahudi walitaka Paulo ahukumiwe.

**Festo alimkumbusha Agripa sheria ya Kirumi. Kamilisha mambo aliyomwambia Agripa katika sentensi ifuatayo hapo chini:**

**SHERIA YA KIRUMI**

Hakuna mshtakiwa ye yote ahukumiwaye kabla ya kukutana na washtaki wake uso kwa uso na kupewa nafasi ya ______________________ kuhusu ______________________ aliyofanyiwa.

Piga mstari chini ya sababu ya Festo kumtaka Agripa kumsikia Paulo.

1. Festo alitaka kumhukumu Paulo kufa.

2. Festo alitaka kujua jambo la kumwandikia Kaisari.

3. Festo alitaka kusikia habari za Yesu Kristo.

Tazama picha hiyo hapo chini. Watu waliopo pichani walikuwa watu muhimu sana wakati ule wa Paulo.




Je! unafikiri Paulo alifurahi kupata Liwali Festo nafasi ya kuzungumza nao?

______________________

Kwa nini, au kwa nini hakufurahia?

______________________

______________________

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**Jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi.**

**Yakobo 5:20**

Ukiwashuhudia wengine habari za Kristo jinsi alivyokufa kwa ajili ya dhambi zao, kisha watu hawa wakatubu dhambi zao, kwa Mungu kwa njia ya Kristo, basi umesaidia kumrejeza mwenye dhambi kutoka katika njia ya dhambi zake. Tukimkiri Kristo kuwa Bwana wetu na kutubu dhambi zetu, roho zetu huokolewa na mauti.



# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Sura ya Kumi na Moja

## KUHAKIKISHA AHADI ZA MUNGU

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 27**

Je! umepata kuketi chini na kufikiri jinsi ulimwengu huu ungekuwa kama Mungu hangalijifunua mwenyewe kwetu kwa Neno lake? Hatungejua habari za Mwokozi. Hatungejua ahadi yake ya kutusamehe dhambi au ya uzima wa milele.

Maisha yanakuwa ajabu kwetu tunapotambua ahadi za Mungu. Mwanafunzi mmoja wa Biblia alihesabu ahadi elfu tatu na mia moja katika Biblia. Sisi ambao tu mali ya Bwana tuna nafasi ya kufanya ahadi hizi zake nyingi kuwa zetu.

Mungu hutimiza ahadi zake daima, lakini anatutaka sisi pia kutimiza sehemu yetu. Wakati Mungu anapofanya ahadi katika Neno lake, ahadi hiyo kwa kawaida imegawanywa katika sehemu mbili, sehemu yake na sehemu yetu. Tukitimiza sehemu yetu bila shaka yeye naye atatimiza sehemu yake.

Katika Yohana 1:12 imeandikwa, "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu." Je! sehemu yetu ni nini? Yatupasa kumpokea Yesu, Mwana wa Mungu. Kumpokea maana yake ni kumwamini na kufuata njia yake katika kila sehemu ya maisha yetu. Tukifanya hivyo, Je! sehemu ya Mungu itakuwa nini? Hutufanya kuwa watoto wake mwenyewe.




Katika kisiwa cha Kanda walipitisha kamba chini ya merikebu ili iishikanishe pamoja. Walipunguzaje uzito wa merikebu?

Walitupa vyombo vya merikebu baharini.

Walitupa nanga nyingine baharini.

Angalia jinsi Paulo alivyoweka mfano mzuri melini. Kata maneno yote yasiyo kweli katika alama hii ( ):

Paulo aliwasihi abiria kula (chakula) (dawa). Walikuwa hawajakula kitu kwa muda wa (siku 2) (siku 14).

Paulo alitwaa (mkate) (keki) akala. Walipokwisha kula wote na kushiba, walitupa (ngano) (mizigo) baharini.

Chora mviringo kwa herufi "K" iliyo kando ya sentensi ya kweli na uchore mviringo kwa herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.

K M Kulipokucha walitambua nchi waliyotumainia kufika.

K M Mawimbi yaliinua merikebu yakaipeleka ukongoni mwa nchi kavu.

K M Kulikuwa na watu wachache ambao hawangeweza kujifikisha nchi kavu salama.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"...huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi." Warumi 4:21**

Mungu anaweza kufanya na kutimiza kila anayoahidi. Paulo alikuwa na hakika juu ya jambo hili. Wewe je?

Katika somo hili tunasafiri na Paulo kuelekea Rumi na tutajifunza jinsi Paulo alivyoamini ahadi za Mungu.

Paulo pamoja na wafungwa wengine walianza safari yao ya kwenda Rumi katika mwezi wa Septemba. (Wakati mwalimu wako anapokusimulia hadithi hii, utataka kutazama ramani yako na kufuata safari hii ya kusisimua.)

Akida ambaye wafungwa walikuwa mikononi mwake aliitwa Yulio na alimtendea Paulo mambo mema. Wakati merikebu ilipofika Sidoni, Yulio alimruhusu Paulo kwenda kuwatembelea marafiki zake pale.

Upepo ulikuwa mkali sana kwa hivyo merikebu ilisafiri polepole kupitia bandari kadha mpaka wakafika mahali paitwapo Bandari Nzuri. Paulo alimshauri Yulio kwamba ingekuwa hatari kwao kusafiri kutoka Bandari Nzuri, lakini nahodha wa merikebu, akijua ya kwamba Bandari Nzuri haikuwa mahali pazuri, aliamua kusafiri mpaka Foinike. Labda Paulo alikuwa amepokea ujumbe kutoka kwa Mungu uliosema kwamba merikebu ile ingekabiliwa na shida kama wangesafiri. Biblia yetu haitwambii cho chote juu ya jambo hilo. Upepo ulipozidi kuvuma kwa nguvu waliacha merikebu yao kupelekwa nayo kwa sababu hawakuweza kushindana nayo.

Walifika katika kisiwa cha Kanda wakataka kuipeleka merikebu ukingoni na wakajaribu kukaza kwa kupitisha kamba chini yake. Lakini bado walipigwa sana na tufani, basi siku ya pili yake walianza kutupa shehena baharini. Siku ya tatu, tufani iliongezeka sana hata wakatupa vyombo vyao vyote baharini. Walifanya hivyo ili merikebu ingepungua uzito wake na kutozama.

Abiria waliokuwamo merikebuni walikuwa hawajakula chakula kwa muda wa siku kumi na nne kwa hivyo Paulo aliwasihi kula. Yeye mwenyewe alitwaa mkate, akamshukuru Mungu mbele yao wote, akaumega, akala. Walipokwisha kula wote chakula cha kutosha, walitupa ngano baharini kupunguza shehena ya merikebu.

Mungu alimwahidi Paulo ya kwamba angefika Rumi na Paulo aliamini ahadi ile. Paulo alijua kwamba imani yake na ya wale waliokuwa pamoja naye merikebuni ilipaswa kuwa thabiti. Mungu alikuwa amemwambia kwamba merikebu ingezama, lakini watu wote wangekuwa salama. Baadhi ya mabaharia walifikiri kwamba wangekuwa salama na kwenda nchi. Walianza kushusha mashua baharini ili wangeweza kupiga makasia bila kujali wenzao. Walikuwa wakijifikiria hali yao wenyewe. Paulo aliona mambo hayo waliyokuwa wakifanya, akawaambia wasitoroke bali wakae mle ndani ya merikebu kama walitaka usalama. Mabaharia walikata kamba za mashua, wakaziacha kuanguka. Kisha wakawasaidia wengine. Baadhi ya askari walipanga kuwaua wafungwa kwa sababu waliogopa kwamba wafungwa wale pengine wangeogelea na kutoroka. Lakini Yulio ambaye hakutaka Paulo kufa aliwazuia kutimiza mpango huu wao. Watu ambao waliweza kuogelea waliambiwa wajitupe baharini na kuogelea hadi nchi kavu, na wengine walishika vipande vya mbao vya merikebu vilivyopasuka, wakasukumwa-sukumwa na mawimbi mpaka nchi kavu. Watu wote walifika nchi kavu salama kama Mungu alivyoahidi. Daima Mungu hutimiza ahadi zake.



WATU WOTE WAKAPATA KUFIKA NCHI KAVU SALAMA

**KAZI YA KUFANYA**

Paulo alikaa kifungoni kwa muda wa miaka miwili. Sasa walisafiri kwenda Rumi kuhukumiwa na Kaisari. Yeye pamoja na wafungwa wengine walikabidhiwa mikononi mwa Yulio aliyekuwa akida wa Kirumi. Paulo alimwambia mwenye merikebu wasisafiri.

Chora mviringo kwa picha ya nanga iliyo mbele ya sentensi ya kweli.

Mwenye merikebu alichagua kutumia wakati wa baridi katika Badari Nzuri kama Paulo alivyomwambia kufanya.

Ingawa Paulo alionya kwamba ingekuwa hatari na safari, mwenye merikebu alisafiri kwenda Foinike.

Paulo alimwambia mwenye merikebu kuendelea na safari mara tu upepo wa kusini ungeanza kuvuma.

Piga mstari chini ya jibu la kweli la kila swali hapo chini.

Merikebu haikuweza kushindana na upepo. Je! mabaharia walifanya nini?

Walisafiri kwenda nchi kavu.

Waliiacha kuchukuliwa na upepo.

Waliwasha moto
Waliwachukia Paulo na wengine.

3. Ni kitu gani kilichomzonga-zonga Paulo mkononi?
ndege nyoka

4. Watu walipoona kitu hiki kilizonga-zonga mkononi mwa Paulo, Je! walifikiri Paulo alikuwa nani?
mchawi mwuaji

5. Walipoona kwamba hakuna dhara lo lote lililompata Paulo, walimfikiria kuwa nani?
mungu malaika

Paulo alimshukuru sana kwa ajili ya ukarimu wa wenyeji wale. Andika majibu ya maswali yafuatayo:

1. Je! Paulo alimfanyia Publio, mkuu wa kisiwa hiki jambo gani.

______________________________

______________________________

2. Je! Paulo aliwafanyia wengine waliokuwa katika kisiwa hiki jambo gani?

______________________________

______________________________

3. Wenyeji waliwapa Paulo na wenzake vitu gani wakati walipokuwa wakiondoka?

______________________________

______________________________

Paulo aliwaambia Wayahudi wa Rumi sababu iliyomfanya kuwa huko. Kata maneno yaliyo katika alama hii ( ) ambayo Paulo hakuwaambia Wayahudi wale.

"Sikufanya neno kinyume cha watu wetu. Lakini nililetwa kama (mfungwa) (mtumwa) kutoka (Bandari Nzuri) (Yerusalemu), nikatiwa katika mikono ya (Wayunani) (Warumi). Walipo-niuliza-uliza, hawakuona sababu yo yote kwangu kuuawa, lakini kwa sababu (Warumi) (Wayahudi) walinichukia, na kusema maneno yasiyo ya kweli juu yangu, nilitaka rufani kwa Kaisari. Niliwaita niwaone na kusema nanyi kwa sababu (nimefungwa kwa minyororo) (nitaachiliwa karibuni) kwa ajili ya Kristo ambaye ni tumaini la Israeli."

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, wapendeni adui zenu, watendeni mema wale ambao wawachukia ninyi." Luka 6:27**

Jambo hili ni gumu sana kwetu kufanya. Je! unakasirika mara kwa mara wakati mtu anapokuchukia? Yesu anakwambia kufanya nini? Huwezi kutii amri za Yesu wewe mwenyewe. Inakupasa kuendelea kumwomba Bwana kukuondolea chuki na ujeuri wako wote. Bwana alimfanyia mtume Paulo hivyo. Atakufanyia wewe pia ikiwa Yesu ni Mwokozi wako na kuishi haki mbele zake.



**VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**

**MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU**

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved.

**Sura ya Kumi na Mbili**

## JINSI YA KUWATENDEA MAADUI

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 28**

Jifanye kana kwamba ulikuwa mmojawapo wa wafungwa waliokuwa pamoja na Paulo wakati merikebu yao ilipovunjika. Hapa pana njia ambayo ungesimulia hadithi juu ya mambo yaliyofanyika.

Merikebu yetu ilivunjika vipande vipande. Askari wangalituua sisi kwa sababu waliogopa kwamba tungeogelea na kukimbia. Lakini Yulio hakuwaruhusu kutimiza mpango huo wao kwa sababu ya Paulo. Sisi sote tuliogelea mpaka nchi kavu, na kama vile Paulo alivyosema, hakuna mtu hata mmoja aliyeangamia. Tulisikia baridi mno na nguo zetu zilikuwa majimaji wakati tulipokuwa tukipanda ufuoni mwa bahari. Nchi hii kavu tuliyofika ilikuwa kisiwa cha Melita. Tulikaribishwa kwa fadhili zisizokuwa za kawaida. Wenyeji wa kisiwa hiki waliwasha moto na sisi sote tukasimama karibu sana na moto huo kuota.



Paulo na wengine walisaidia kukusanya mzigo wa kuni wa kuweka motoni. Wakati Paulo alipoweka ukuni mmoja motoni, nyoka alitoka

ndani ya ukuni huo kwa ajili ya ule moto, akamzonga-zonga mkononi. Watu walipoona jambo hilo waliambiana wao kwa wao ya kwamba Paulo, bila shaka alikuwa mwuaji. Sisi sote tulishangaa wakati Paulo alipomtukusha yule nyoka kutoka mkononi mwake, na mkono wake haukufura wala haukupata madahara yo yote. Basi, watu walianza kuambiana sasa ya kwamba Paulo alikuwa mungu.

Mkuu wa kisiwa hiki aliitwa Publio. Babaye Publio alikuwa mgonjwa kwa muda mrefu, na Publio alipomwambia Paulo habari hii, Paulo alikwenda kumtembelea. Wakati Paulo alipokuwa huko aliomba, akaweka mikono yake juu ya baba wa Publio na ugonjwa wake ukamwacha. Pia, Paulo aliwaponya watu wengi waliokuwa wagonjwa.

Tulikaa katika kisiwa hiki kwa muda wa miezi mitatu. Kulikuwako pale merikebu nyingine ambayo ilikaa pale wakati wa baridi. Ilikuwa imetoka Iskanderia. Yulio alifanya mpango wa sisi kusafiri kwenda Italia katika merikebu ya Iskanderia. Tuliingia katika merikebu hii, na kabla ya kuondoka, wenyeji wa kisiwa hiki walituletea vitu tulivyokuwa na haja navyo pamoja na zawadi. Wenyeji hawa walikuwa wakarimu sana kwetu wakati tulipokuwa katika kisiwa hiki.

Tulisimama mara mbili katika safari yetu ya kwenda Rumi. Mahali pa kwanza tuliposimama paliitwa Sirakusa, kisha tukasimama Regio.

Baada ya muda mfupi tuliwasili Puteoli. Hii ni bandari kubwa ambapo merikebu zote kubwa zilisimama ili kupakua shehena zao. Kutoka hapo tungetembea kwa miguu mpaka Rumi.

Tulikaa Puteoli kwa muda wa wiki moja. Wakristo wa pale walikuwa wamekwisha kusikia habari za Paulo na wengi wao walikuja kumtembelea Paulo na kuzungumza naye.

Baada ya wiki ile moja kwisha, tuliondoka, tukaanza kutembea kwa miguu kwenda Rumi. Tulipokuwa kilometa sitini na tano kutoka mji wa Rumi, Wakristo wengi kutoka Rumi walikuja kumlaki Paulo. Walikuwa wamekwisha kusikia habari ya kuja kwake na walitaka kumjua. Jambo hili lilimtia Paulo moyo alipojua kwamba Wakristo hawa walipendezwa sana naye hata wakajitoa kutembea umbali huo wote ili wapate kumwona. Nilitambua ya kwamba Wakristo wana upendo kati yao na pia kwa watu wengine. Wakristo wengine walimlaki Paulo karibu na mji wa Rumi.

Wakati tulipofika Rumi, Yulio aliwapeleka wafungwa wote ngomeni. Sisi sote tulipelekwa ngomeni isipokuwa Paulo. Nilisikia ya kwamba aliruhusiwa kukaa nyumbani kwa Mkristo mmoja, lakini alikuwa amefungwa kwa minyororo pamoja na askari wa kumlinda usiku na mchana wote.

Mfungwa ambaye alianza kusimulia hadithi hii sasa ilimbidi kwenda ngomeni, mbali na Paulo. Luka ataendelea kutusimulia hadithi hii.

Paulo alikaa nyumbani mwa Mkristo mmoja, na ingawa alilindwa usiku na mchana, aliruhusiwa kutembelewa na wageni. Watu wengi walikuja kuzungumza naye. Baada ya kukaa Rumi kwa siku tatu tu, Paulo aliwaita wakuu wa Wayahudi akawaeleza sababu iliyomfanya kuletwa Rumi. Je! unajua ni kwa nini Paulo alipelekwa Rumi? Ikiwa unakumbuka sababu hiyo, shiriki na wengine ambao hawajui. Lakini ikiwa hukumbuki, rudia tena masomo yako mpaka upate jibu.

Paulo aliwaeleza Wayahudi hawa mafundisho ya Agano la Kale juu ya Kristo. Wengine waliamini maneno yake ya kuwa ni ya kweli. Lakini wengine wengi hawakuyaamini. Paulo aliwaambia watu wale ambao hawakuamini ya kwamba angepeleka ujumbe ule wa wokovu kwa watu wa Mataifa.

Paulo alifungwa miaka miwili. Aliruhusiwa kupanga nyumba ya kukaa wakati wa miaka hiyo miwili, lakini sikuzote alifungwa kwa minyororo na askari aliyemlinda. Wakati alipokuwa katika nyumba ile aliyopanga, aliyaandikia makanisa aliyoanzisha barua. Pia, alikuwa na wageni wengi waliomtembelea na alimwambia kila mmoja wao habari za wokovu wa Kristo.

Paulo hakutumia wakati wote kujisikitisha. Alikuwa mwema hata kwa watu ambao walimchukia. Alijua ya kwamba ilikuwa muhimu sana kwa watu wote kujua upendo mkuu wa Mungu kwa kumtuma Mwanawe ulimwenguni kufa msalabani kwa ajili yetu. Kristo alituvuta sisi sote kwake kwa upendo wake. Huo ndio namna ya upendo anaoweza kujaza moyoni mwako ili upate kuwapenda wengine wanaokuchukia.

Je! una furaha ya kwamba Mungu anakupenda? Umefurahi ya kwamba Kristo anaweza kukufanya kuwa kama yeye? Ukimwomba ataujaza moyo wako kwa upendo wake na kukusaidia kuwa mwema kwa watu wote hata kwa wale wanaokuchukia. Mungu wetu ni mkuu na tena ni wa ajabu!

**KAZI YA KUFANYA**

Mungu aliokoa tena maisha ya Paulo. Wakati huu alimwokoa Paulo katika bahari iliyochafuka na kuvunja merikebu waliyokuwa wakisafiria. Baada ya muda mfupi Paulo na abiria wengine walitambua kwamba walikuwa katika kisiwa cha Melita. Piga mistari chini ya majibu ya kweli ya maswali yafuatayo.

1. Hali ya hewa ilikuwaje?

ya joto kidogo

ya mvua na baridi

2. Wenyeji walikuwaje wakarimu kwa watu wale waliotoka melini?

kando yake. Ukihitaji kutafuta majibu ya maswali haya, soma Matendo 21:3-6.

"Wakati nilipokuwa katika mji wa __________ ilinibidi kupeleka kesi yangu mbele ya liwali mpya. Jina la liwali huyu mpya liliitwa ________. Nilikuwa nimekwisha kukaa gerezani miaka miwili. Sasa wakuu wa Wayahudi walikuwa bado wakijaribu kunifanya niuawe. Kisha nilipeleka kesi yangu mbele ya mfalme, aliyeitwa.. Yeye pamoja na Bernike dada yake walisikia maneno yangu."

Tafuta mji huu katika Ramani yako na uandike namba 3 kando yake. Ukihitaji kuhakikisha majibu yako, soma Matendo 25:13-22.

"Nilitaka rufani kwa Kaisari ili aweze kusikia kesi yangu, kwa hivyo Festo alinituma Rumi. Safari ya kwenda Rumi ilikuwa ndefu na mambo mengi ya ajabu yalinifanyikia njiani. Nilimwambia nahodha wa merikebu tukae pale katika __________ __________ wakati wa baridi. Lakini yeye hakunisikiliza, basi tukaanza safari ya kwenda Foinike. Tulipokuwa njiani, dhoruba kali ilitujia. Baada ya siku nyingi, merikebu yetu __________ na sisi sote tukafika salama katika kisiwa cha __________."

Tafuta kisiwa hiki katika ramani yako halafu andika namba 4 hapo. Maelezo juu ya safari hii ya ajabu yanapatikana katika Matendo 27:8-12, 41 na Matendo 28:1.



# VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA TATU

# PAULO, MJUMBE WA MUNGU

Africa Coodinated Curriculum for Bible Study

J1 - 3PS

© Copyright 1988, Baptist Publications House, Nairobi, All Rights Reserved

Somo la Kumi na Tatu

## SOMO LA MARUDIO

MASOMO YA BIBLIA: Maandiko yote ya masomo ya masomo kumi na mawili yaliyopita.

VIFUNGU VYA KUKUMBUKA

Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe. Matendo 3:19a

Mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa, mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu. Wakolosai 1:10

Nitamwimbia Bwana maadamu ninaishi; nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai. Zaburi 104:33

Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani. Yohana 5:24

Kwa maana mimi, Bwana, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; mimi nitakusaidia. Isaya 41:13

Nimemweka Bwana mbele yangu daima, kwa kuwa yako kuumeni kwangu, sitaondosha. Zaburi 16:8

Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, "Mimi hapa, nitume mimi." Isaya 6:8

Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake. Wafilipi 1:29

Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?
Waraka kwa Waebrania 13:6

Jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi.
Yakobo 5:20

Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi
Warumi 4:21

Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi. Luka 6:27

Tumefikia mwisho wa mafunzo yetu juu ya Paulo. Tumemfuata tangu mwanzo wa maisha yake ya Kikristo wakati alipoona maono njiani akienda Dameski, mpaka safari yake ya mwisho ya kwenda Rumi ambako alikufa. Paulo anaweza kutufundisha mambo mengi kutokana na maisha yake ya Kikristo ambayo ni ya ajabu.

Labda tutaweza kukosa kuona wakati wa hatari ambao Paulo aliona katika masomo haya ambayo tumejifunza. Maisha yetu yanaweza kuwa ya kadiri tu, na tunaweza kuona kwamba hakuna jambo lo lote la kusisimua ambalo linatufanyikia. Bila shaka hatutaitwa kuteseka kwa ajili ya Bwana wetu Yesu kama Paulo alivyofanya mara kwa mara. Lakini hadithi hizi juu ya Paulo zinaweza kutufundisha mengi kuliko maisha yake.

Paulo anatufundisha kwa kutuonyesha jinsi ya kuishi maisha mema siku ya leo. Sisi tukiwa kama Paulo, ni lazima tumpe Kristo nafasi ya kwanza maishani mwetu kama vile alivyofanya. Tunapofanya hivyo, Bwana atataka kututumia kama alivyotumia Paulo. Atatupa nafasi za kushiriki imani yetu na kuwahubiria watu wengine wengi Injili yake. Tunaweza kupata ahadi za Mungu maishani mwetu na kuona Neno lake kuwa ni la kweli daima. Tunaweza hata kutumia upendo ule ambao Yesu alijaza mioyoni mwetu kuwatendea maadui zetu mambo mema kama vile Paulo alivyofanya.

Yesu anataka kuwa mfano wa kwanza wetu kwa maisha, lakini pia mara kwa mara tunawaona watu kama Paulo wanaoweza kutupa mfano mzuri wa kuishi maisha mema ya Kikristo. Tukitumia mambo ambayo Paulo ametufundisha kwa kujifunza habari kuhusu maisha yake, basi tutaona ya kwamba tunaishi karibu na Bwana wetu Yesu Kristo.

Tutarudia hadithi kadha tulizojifunza katika masomo yote ya kitabu hiki ili yatusaidie kukumbuka hadithi fulani juu ya Paulo, na kukumbuka mambo mengine aliyotufundisha. Itakuwa jambo jema kuona kwamba tunaweza kukumbuka kadiri gani habari juu ya Paulo!

Jaribu kujibu kila swali bila kutafuta jibu katika Biblia. Maikiliza Paulo akitwambia mambo haya ya ajabu.

**KAZI YA KUFANYA**



"Nilikuwa njiani kwenda __________ kuwatesa Wakristo. Kwa ghafula __________ kutoka mbinguni ikaniangaza kote kote na kunipofusha macho. Sauti iliniita kwa jina langu la Kiyahudi, '_______, _______, mbona waniudhi?' Sauti hii ilikuwa ya _______ aliyekuwa na kazi aliyotaka nifanye. Ni hapa ndipo nilipogeuka kuwa Mkristo." Sasa, katika ramani yako unaweza kuandika namba 1 kando ya mji ambao Paulo aligeuzwa kuwa Mkristo. Hadithi hii inapatikana katika Matendo 9:3-9.

"Mambo mengi ya ajabu yalinifanyikia katika safari zangu. Nilikutana na watu wengi walionitakia baraka za Bwana. Siku moja marafiki wengine walinionya nisiende mji wa __________. Watu hawa walikuwa marafiki zangu wa mji wa __________. Kabla ya kuwaacha na kuendelea na safari yangu, tulipiga magoti pwani __________." Tafuta



mji huu katika ramani yako, kisha andika namba 2